MAELEZO YA MWEZESHAJI

Kuwa kwenya mahusiano na watu walio kuzidi umri

Maelezo muhimu

Mwaise anafikiria kuwa kwenye mahusiano na mtu aliye mzidi umri lakini hana uhakika.
Je, nini anapaswa kufanya?

Kuwa na mahusiano na mwanaume au mwanamke mwenye umri mkubwa zaidi kuliko wewe – Inawezekana unapewa zawadi nyingi na unapelekwa sehemu za kifahari lakini kumbuka:

- **Wanaweza kutegemea au kulazimisha uwapatie vitu usivyotaka kuwapatia, kama kufanya mapenzi.**
- **Kunauwezekano mkubwa kwamba watataka kusikilizwa wao tu, kwa hiyo itakuwa vigumu kwako kuzungumzia kuhusu matumizi ya kondomu.**
- **Kuna uwezekano mkubwa kwamba wanaweza wakawa wanaishi na virusi vya ukimwi. Kama hutakubali kutumia kondomu basi utajiweka kwenye hatari ya kupata virusi vya ukimwi na magonjwa mengine ya ngono.**
- **Wanaweza wakawa wanafanya ngono na watu wengine wenye umri kama wako, hii huongeza hatari ya maambukizi zaidi ya magonjwa ya ngono.**
- **Unaweza hisi ukotayari, lakini matarajio yao yanaweza yakawa tofauti na yako.**
- **Kwakuwa marafiki zako wanamahusiano na watu wazima, bado utapaswa kufanya maamuzi sahihi.**

Mawazo ya mjadala

Ni nini ambacho wewe au kikundi chako mnafikiria kuhusu mahusiano ya watu wenye umri tofauti kabisa? Labda hujawahi kulifikiria hili kabla. Haya ni maswali ya kufikiria binafi au kujadili kwenye kikundi chako.

- **"Blessers" ni mfano wa jina ambalo hupewa mwanaume anaye toka na wasichana wado sana kumliko, "Ben 10's" nimfani wa jina analipewa kijana mdogo anaye toka na wamama wenye umri mkubwa kumliko. Je kunamajina mengine ambayo hutumuka mahali unapoishi? Unaposikia watu wakiitwa majina haya, inakupa mtazamo gani?**

MAELEZO YA MWEZESHAJI

Kikundi kinaweza kufikiria majina kama; sugar daddy/sugar mama/fataki/kienten nk. Umegundua kuwa maranyingi majina haya huonyesha kwamba kutoka na mtu mkubwa zaidi kuliko wewe ni kama bahati. Sawasawa tu na kumuita mtu mjomba inakaa nikama mtu atakaye kuangali au kukuhudumia vizuri au mtu utakaye takiwa kumuheshimu na kufanya kile atakacho sema.

Unapojadili kuhusu hili unaweza kuanza kuchunguza kuhusu nguvu ya usawa wanayoweza kuipendekeza. Kwa mfano, kama unamuona mtu Fulani kuwa ni Baraka kwako basi utataka kumhudumia kiutofauti kwa sababu una bahati kuwa naye na hungependa kumpoteza.

- **Unadhani ni sababu gani ambazo hufanya vijana wa kike na vijana wa kiume kuwa kwenye mahusiano na watu wazima?**

MAELEZO YA MWEZESHAJI

Maranyingi wengi huvutiwa na pesa ambazo watu hawa huwa nazo na zawadi ambazo huwapatia. Pia inaweza ikawa vijana hufikiri kutoka na watu wenye umri mkuwa kuwaliko inaweza kuwafanya waonekane kuwa ni wajanja zaidi; kwamba wakiwa nao wanaweza kwenda kunywa au kuhudhuria sherehe za kifahari. Jadili hizi sababu na endelea kuchunguza ni nini sababu na hofu zinazoweza kuwepo – kwamfano kama itapelekea mmojawao kuwa na nguvu na maamuzi zaidi kuliko mwingine.

- **Kma ungekuwa unatoka na mtu aliye kuzidi umri ambaye anakupatia msaada wa kifedha, unadhani hili lingeathiri vipi mahusiano yako? Fikiria kuhusu faida na hasara ambazo zinaweza kupatikana.**

MAELEZO YA MWEZESHAJI

Kikundi kinaweza kusema kuwa watu walio wazidi umri wanauwezo wa kuwapatia wenza wao vile vitu wanavyo hitaji. Wanaweza kuwalipia ada au safari. Hii huweza kuwafanya kuwa wenye shukrani au wanaweza kujikuta wakihisi kuwa na ukaribu na wenza wao au hata kuwapenda zaidi.

Ingawa, wanatakiwa pia kutumia mudawao kuelezea vile kupokea zawadi kunaweza kusababisha ugumu zaidi wa kumkatalia mwenza wako vitu fulani mbeleni. Inaweza kuwafanya wahisi kama wana dena kwa wenza wao ambapo itawapatia uzito wa kukataa kufanya mapenzi au kusisitiza kutumia kondom.

- **Je, unafahamu kwamba wanaume na wanawake wazee wanauwezekano mkubwa zaidi wa kuwa na VVU au magonjwa mengine ya ngono kuliko vijana, kwasababu wamekuwa wakifanya mapenzi kwa muda mrefu? Je, hili linaweza kubadilisha mtazamo wako kuhusu kutoka na watu walio kuzidi umri Zaidi?**

MAELEZO YA MWEZESHAJI

Dhumuni la mazungumzo haya si kuwanyanyapaa walio athirika na virusi vya ukimwi au magonjwa mengine ya ngono, ila ni kuchunguza hatari zinazoweza kusababishwa kwa kutoka na watu walio kuzidi ummri. Pale panapokuwa na utofautiano wa kimaamuzi katika mahusiano, Unaweza usiwe na nguvu/ sauti ya kuamua kuhusu matumizi ya kondom na uhuru wa kufanya mapenzi. Huo ni wakati ambao uko hatarini zaidi. Wengi wanaweza kufikiria pia kama wangependa kuwa kwenye mahusiano ambayo hawana nguvu ya kuamua kufanya mapenzi salama.

- **Mahusiano ya wengi ambao wametofautiana miaka, ni yale ya watu ambao hawakufunga ndoa. Unadhani nini kinaweza kuwapata vijana wadogo walio kwenya mahusiano ya aina hii?**

MAELEZO YA MWEZESHAJI

Ndoa si tiketi ya mahusino salama na yenye afya. Lakini nivizuri kwa wapenzi kukubaliana kwakile wanachokitaka katika mahusiano yao, ikiwemo kama ni sawa kutembea na watu wengine. Vikundi lazima vifahamu kwamba kuwa na wenza wengi huongeza uwezekano wa kupata maambukizi ya virusi vya ukimwi. Kama mpenzi wako ni mtu aliye kuzidi umri na anawapenzi zaidi ya mmoja, hatari ya kupata maambukizi ya magonjwa ya ngono huwa juu zaidi. Uwazi/ukweli na kushirikiana majukumu na maamuzi ni muhimu kwenye mahusiano ya wazi, hasa tunapozungumzia kufanya ngono salama.

Habari Zaidi

Ishara za maonyo ya mahusiano yasiyo salama
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/martha

Jinsi ya kukataa kufanya ngono
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/chipo

Kuongelea kuhusu virusi vya ukimwi na mwenzi wako
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/lineo

Ngono bila kondomu
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/spijo

Njia mbalimbali za uzazi wa mpango
https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/babalwa

Young Voices ni kikundi kinacho jadili kuhusu mijadala mbalimbali ya afya ya uzazi na kufanya ngono salama. Unaweza kupata taarifa za kutosha kwenye: **https://www.avert.org/hubs/young-voices/swahili/**

March 2021